ictj chapisho fupi

ICTJ Justice Truth Dignity

Agatha Ndonga
Ruben Carranza
December 2019

Tume Ya "Building Bridges" Yaweza Kuvunja Michakacho Ya Ufisadi Na Vurugu Za Kisiasa Nchini Kenya?

Kenya ni mojawapo ya nchi za kwanza kujumuisha katika jukumu la tume ya ukweli uchunguzi wa ufisadi wa kimfumo iliyofanywa na serikali za zamani na kuwataja wale ambao wanapaswa kuwajibishwa. Katika ripoti yake, Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano ya Kenya (TJRC) ilipata kwamba "ufisadi umeenea nchini Kenya" na kwamba "kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya ufisadi na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu."[1] TJRC ilipata kwamba ufisadi "una athari kubwa kwa vikundi vilivyo hatarini kama vile watu maskini, watu asilia, wanawake, watoto, watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI, wakimbizi na wakimbizi wa ndani kwa ndani, na wafungwa.[2] "Theluthi moja ya bajeti ya serikali ya Kenya, au karibu bilioni 6 za Marekani, hupotea kutokana na ufisadi kila mwaka.[3] Kwa upande wake, ukosefu wa usawa na umaskini uliosababishwa au kuzidishwa na ufisadi mkubwa ulioko nchini Kenya huchangia vurugu za kisiasa. "Binadamu wameuawa, kudhulumiwa na ukiukwaji wa aina zingine za haki za binadamu," TJRC iliripoti, "kwa sababu ya juhudi zao za kupambana na ufisadi."[4] Kati ya mwaka 1997 na Septemba 2013, Kenya imeshuhudia zaidi ya visa 3,500 vilivyorekodiwa vya vurugu za kisiasa.[5]

Kutokujali kwa kiwango kikubwa nchini Kenya kuna matokeo mengine: Kumepotosha maadili ya Wakenya, haswa vijana (watu kati ya miaka 18 na 35), ambao ni asilimia themanini (80%) ya idadi ya Wakenya.[6] Katika utafiti wa 2016 uliofanywa na Chuo Kikuu cha Aga Khan nchini Kenya, asilimia arobaini na saba (47%) ya vijana Wakenya waliohojiwa walisema ya kwamba waliwahusudu watu wanaojilimbikizia utajiri kwa njia ya wizi wa rasilimali za umma, ilhali asilimia nyingine thelathini na tano (35%)

MEZA YA YALIYOMO

Kutowajibika/Kutokujali na Wanasiasa Tajika wa Kenya 2
Jinsi Ufisadi Unavyoendelea Kuchochea Ghasia za Kisiasa 4
Kuendeleza Udhalimu wa Ardhi kupitia Ufisadi 6
Kujifunza kutoka kwa Nchi Zingine 7
Kuenda Zaidi Ya "Ujenzi Wa Madaraja" 8

1 TJRC Kenya, "Report of the Truth, Justice and Reconciliation Commission, Volume 4" (2013), p.56. Website: http://knchr.org/Portals/0/Reports/TJRC_Volume_4.pdf.
2 Ibid.
3 Duncan Miriri, "Third of Kenyan Budget Lost to Corruption: Anti-graft Chief," Reuters, March 10, 2016. Website: www.reuters.com/article/us-kenya-corruption/third-of-kenyan-budget-lost-to-corruption-anti-graft-chief-idUSKCN0WC1H8.
4 TJRC Kenya, "Report of the Truth, Justice and Reconciliation Commission, Volume 4" (2013), p. 56. Website: http://knchr.org/Portals/0/Reports/TJRC_Volume_4.pdf.
5 Brigitte Rohwerder, *Conflict Analysis of Kenya* (Birmingham, UK: GSDRC, University of Birmingham, 2015).p. 3. Website: www.gsdrc.org/wp-content/uploads/2015/12/KenyaConflictAnalysis.pdf.
6 Alex O. Awiti and Bruce Scott, the Aga Khan University, "The Kenya Youth Survey Report" (2016). p. 1. Website: www.aku.edu/eai/Documents/kenya-youth-survey-report-executive-summary-2016.pdf.

walisema kwamba wako tayari kuchukua au kutoa hongo. Nusu ya waliohojiwa walisema "hawatakuwa na shida ya kukwepa ushuru au kuchukua hongo iwapo hawatafungwa gerezani."[7]

Mnamo mwaka wa 2018, Rais Uhuru Kenyatta na Waziri Mkuu Wa Zamani aliye pia Kiongozi Wa Upinzaji Wa Kisiasa (sasa mshirika wa ndani wa kisiasa) Raila Odinga kwa pamoja walizindua mpango unaojulikana kama "Building Bridges to a New Kenyan Nation Iniative" — ili kurejesha amani na uwiiano nchini Kenya, ambao sasa unajulikana kama "the handshake." Kulingana na waraka huo uliozinduliwa na pande hizo mbili, mpango huo unakusudiwa kuleta "…mfumo wa heshima kwa wote, ustawi na usalama."[8] Nakala hiyo inaashiria masuala tisa (9) ambayo mpango huo utashughulikia ili kuunda nchi/Taifa yenye umoja kwa Wakenya wa sasa na wa siku za baadaye. Mojawapo ya masuala hayo ni ufisadi, ambao uilielezewa kama "tishio linalozindikana Kenya."[9]

Lakini wakati serikali imechukua hatua kushughulikia ufisadi, ukiwemo pia Mpango wa "Building Bridges Initiative," (BBI) hatua hizi kulingana na Wakenya zinapigwa vinywani tu hivo basi kuchangia kidogo kubadilisha maoni kwamba ufisadi bado umekita mizizi na umeenea kwenye jamii mzima ya Kenya. Nakala hii kwa hivyo inazingatia kiwango cha kutowajibika na kutojali ufisadi nchini Kenya, jinsi ufisadi unavyochochea na kuchangia machafuko ya kisiasa na ukiukaji wa haki za umiliki wa ardhi, na jinsi Kenya inaweza kujifunza kutoka kwa nchi nyingine mbinu za kuunganisha au 'ujenzi wa madaraja' kati ya wanasiasa tajika na kulinda haki za raia wake kwa umakinifu.

Kutowajibika/Kutokujali na Wanasiasa Tajika wa Kenya

Mpango wa "Building Bridges Initiative" sio mara ya kwanza ya wanasiasa tajika wa Kenya, iwe kikundi kimoja au vikundi kadhaa vya pamoja, wameahidi kukomesha ufisadi. Majaribio haya ya kupambana na ufisadi yaliyoongozwa na wanasiasa tajika yamekuwa na matokeo sawa: Waliacha mfumo wa upendeleo wa na ukabila uliowaweka viongozi mamlakani, kuhakikisha kutowajibika/kutokujali kwa viongozi katika viwango vya juu, na hivyo kuwaruhusu kuendeleza au kujinufaisha na shughuli za uporaji (kwa mfano, hongo na ushawishi), uporaji wa rasilimali za umma ikiwemo ardhi/mashamba na, na kulinda mali walizozipata kwa njia ya ufisadi. Wanasiasa tajika wa nchini Kenya walipochukua utawala au madaraka kutoka kwa wakoloni wa Uingereza, walidumisha historia ya ukoloni wa Uingereza wa ufisadi na ukandamizaji. Kama ilivyoelezewa na mwanahistoria mmoja nchini Kenya:

> Ukoloni ulichangia sehemu yake katika kukosekana kwa usawa nchini na umaskini kwani ulikuza tofauti za vijijini-mijini, kikanda na tofauti za matabaka katika maendeleo. Matokeo yake ni, utata ulioenea enzi za ukoloni wa Kenya umethibitishwa. Hii ni pamoja na utata katika uhusiano wa kijamii wa uzalishaji kati ya ubepari wa kimataifa na wa nyumbani, kati ya maskini na ubepari, na kati ya matajiri na wafanyikazi. Kama jimbo la wakoloni, serikali

7 Ibid.
8 "Building Bridges to a New Kenyan Nation," March 9, 2018, p. 1. Website: www.president.go.ke/2018/03/09/building-bridges-to-a-new-kenyan-nation/.
9 Ibid., p. 6.

Tume Ya "Building Bridges" Yaweza Kuvunja Michakacho Ya Ufisadi Na Vurugu Za Kisiasa Nchini Kenya?

> za baada ya ukoloni zimelazimika kukabiliana na msururu wa utata. Ubepari wa kawaida wa nyumbani huandamana na ufisadi mkubwa ili kumiliki mali na mamlaka. Wanachangia pia ubaguzi wa rangi na mivutano ya kikabila ili kukaa mamlakani.[10]

Hata serikali ya Rais mstaafu Mwai Kibaki, iliyoitoa Kenya kutoka kwa mfumo wa kimabavu wa chama kimoja na ikachaguliwa kwenye jukwaa la kumaliza ufisadi nchini, ilibuni na kuendeleza kashfa kubwa za ufisadi. Wakati wa enzi ya Kibaki, viwango vya ufisadi viliongezeka; kashfa ya Anglo-Leasing,[11] haswa, ilikabili nchi hata kabla kashfa ya Goldberg,[12] ambayo iliathiri wanasiasa maarufu waliokuwa kwenye serikaliya Moi, mtangulizi wa Kibaki kusuluhishwa. Kunukuu ripoti ya Tume ya Uchunguzi kuhusu kashfa ya Goldberg: "Hakuna mtu anayeweza kufikiria juu ya jambo jingine ambalo limechukua muda wa sehemu zote za Serikali; Ofisi ya Rais, Bunge na Mahakama, kuliko kashfa ya Goldberg. Hakuna lolote katika maoni ya umma ambalo limejitokeza kushinda aina za ufisadi kama ya Goldenberg. Maovu ya ufisadi na athari zake mbaya inazochangia na basi kuzikumba jamii zinajulikana dhahiri shahiri".[13]

Kuendelea kwa ufisadi wa kiwango kikubwa, hata baada ya mabadiliko ya awali ya uongozi kutoka kwa Moi kwenda hadi Kibaki, inaonyesha kuwa mabadiliko kutoka kwa utawala wa kimabavu hadi utawala wa kidemokrasia peke yake haitapelekea kupungua kwa ufisadi na uibukaji wa ghasia za kisiasa ambazo huchangiwa na mafisadi. Kwa kweli, mtu anaweza kusema kuwa kinyume kilitokea nchini Kenya: Sasa kwa kuwa mafisadi waliweza kugombania mamlaka ya kisiasa, machafuko makubwa zaidi ya kisiasa yalitokea.

Licha ya kampeni nyingi za kupigana na ufisadi, sheria mpya, na tume ya kupambana na ufisadi iliyoimarishwa, ufisadi unaendelea nchini Kenya kwa kiwango ambacho sio tofauti na hapo awali. Serikali ya sasa imekuwa ikigandamizwa na kashfa kadhaa za ufisadi.[14] Mnamo Januari 2019, Rais Kenyatta na Waziri Mkuu wa zamani Odinga waliongoza kwa pamoja Mkutano wa Kitaifa wa Kupambana na Ufisadi ulioletwa pamoja na Jukwaa la Sekta Kuu, ambao ni mpango wa kupigana na ufisadi. Mkutano huo ulilenga kutafakari na kushirikisha Wakenya juu ya jinsi ya kukabiliana na ufisadi. Waliohudhuria walijumuisha viongozi wa kitaifa, wasomi, wachungaji, na watendaji wa tasnia, na pia vikundi vya wanawake, wanahabari, vikundi vya vijana, na mashirika ya kitaaluma. Dhihirisho la nia njema kati ya viongozi wote wawili juu ya suala hilo umesitishwa, na ufadhili ulioongezeka wa uchunguzi wa kupambana na ufisadi umetambuliwa. Lakini, hata maneno ya viongozi au juhudi za kupambana na ufisadi, pamoja na kuanzishwa kwa BBI yenyewe, yamepunguza ubeuzi na wasiwasi wa wakenya wengi ambao wanaona

10 Peter O. Ndege, "Colonialism and Its Legacies in Kenya," lecture delivered during Fulbright–Hays Group Project-Abroad Program, July 5-August 6, 2009, Moi University, Eldoret, Kenya. Website: https://africanphilanthropy.issuelab.org/resources/19699/19699.pdf.

11 The Anglo-Leasing scandal involved the awarding of over 20 government contracts at inflated costs during the Moi presidency. Several overseas companies, including Anglo Leasing Finance, were implicated. See "Kenyan Taxpayers Robbed of $1 Billion in 'Anglo-Leasing' Scandal," *The Great Rip Off*, https://greatripoffmap.globalwitness.org/#!/case/51.

12 The transactions in the Goldenberg scandal happened from 1990 through 1993 and implicated Moi in a scheme where precious metals from thirdworld countries went through Kenya and were reexported by a company called Goldenberg, which then received subsidies from the state. See Jeevan Vasagar, "Former Kenyan Leader Should Face Corruption Inquiry, Says Report," *Guardian*, February 4, 2016. Website: www.theguardian.com/world/2006/feb/04/kenya.jeevanvasagar

13 Report of the Judicial Commission of Inquiry into the Goldenberg Affair" (October 2005), p. 308. Website: http://kenyalaw.org/kl/fileadmin/CommissionReports/Report-of-the-Judicial-Commission-of-Inquiry-into-the-Goldenberg-Affair.pdf.

14 Jacob Onyango, "15 Mega-Corruption Scandals in Kenya Which Have Never Been Resolved," *Tuko*, 2018. Website: www.tuko.co.ke/274539-15-mega-corruption-scandals-kenya-resolved.html#274539.

juhudi hizi kama siasa tu huku wanasiasa wengine wakipuuza hivi vita dhidi ya ufisadi na kuchochea ghasia za kikabila.[15]

Historia hii ya ufisadi, mizizi yake, na kukita kwake kwa sababu ya ukosefu wa juhudi zozote za uwajibikaji ndizo zilipelekea Michela Wrong katika kitabu chake maarufu na chenye utata nchini Kenya, kuhitimisha, "Nchini Kenya, ufisadi haukomeshwi na mageuzi, unahama tu… [na] chini ya tabaka zote, kifusi kikubwa, na msingi imara ndio husalia: Wakenya na dhana teuka kwao wenyewe. Aina tofauti za ufisadi haziwezi kutengwa na maono ya watu kuwa kama pambano lisilo na huruma, na mapendeleo ya kikabila tu ndiyo yanayotoa matumaini ya kuishi."[16]

Jinsi Ufisadi Unavyoendelea Kuchochea Ghasia za Kisiasa

Mmoja wa maKamishna wa TJRC, Ronald Slye, alielezea kwamba "hakuna shaka kuwa ufisadi uliokita mizizi na unyakuzi wa ardhi kubwa zilihusishwa, na katika visa vingine vilikuwa sababu za moja kwa moja, ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu nchini Kenya."[17] Mzunguko huu wa ufisadi na ukiukaji wa haki za binadamu wakiwepo pia wale walioathiriwa wakati wa ghasia za kisiasa, unaendelea kivipi? Kulingana na Tume ya Uchaguzi ya Kenya, wanasiasa mara nyingi husambaza pesa kama hongo sio tu kwa kununua kura lakini pia kuhamisha wapiga kura katika maeneo ambayo wanaweza kubadilisha matokeo ya uchaguzi.[18] Uhamishaji wa wapiga kura haramu bado ni jambo kutia wasiwasi kwa sababu limetumika kuondoa wapinzani na kuwatisha wafuasi wa wapinzani, haswa wale wanaodhaniwa kama "wageni," na hivyo kuongeza mgawanyiko wa kikabila zaidi na kuongezeka kwa fujo zinazohusiana na uchaguzi au kisiasa.

Vurugu za kisiasa zinazidi kuchukuliwa kama jambo la kawaida wakati wa uchaguzi nchini Kenya. Jambo hilo liliibuka kutokana na kurejea kwa siasa ya vyama vingi mnamo 1991, kulingana na Tume ya Akiwumi.[19] Katika mapendekezo yake, Tume hiyo ilitaka uchunguzi na uwezekano wa mashtaka ya wanasiasa wa juu na viongozi wa serikali kwa jukumu walilochukua katika kuchochea mapigano ya kikabila mnamo 1992 na 1997. Tume hiyo pia iligundua kuwa vijana wa Kenya katika sehemu mbali mbali za nchi walipokea mafunzo ya kijeshi kushambulia "wasiohusika/wageni." Upangaji, ufadhili, na uratibu wa mafunzo haya ulifanywa na wanasiasa ambao walitumia pia polisi na vifaa vya Utawala wa Mikoa wakati huo kuzua vurugu dhidi ya wapinzani wao wa kisiasa.

Kuzuka kwa vurugu kubwa na za kimfumo za baada ya uchaguzi mnamo 2007 na 2008 hazikufanyika bila kutabirika wala kutarajiwa. Inaonyesha jinsi mapigano yanayohusiana na uchunguzi mara kwa mara yanaweza kugeuka kuwa vitendo vikubwa vya kurithia vurugu za kisiasa, bila kulenga tu wapinzani au vikundi vya kisiasa, lakini raia wa kikundi cha utambulisho fulani.[20] Ingawa uchaguzi mkuu mnamo 2013 haukushuhudia vurugu za kisiasa, kwa sababu ya kile kinachoaminika kuwa kizuizi kilichopelekewa na kuwepo

15 Macharia Gaitho, "Politicizing War on Corruption Akin to Fanning Ethnic Violence,"Daily Nation, December 11, 2018. Website: www.nation.co.ke/oped/opinion/Politicising-war-on-graft--akin-to-fanning-ethnic-violence/440808-4889638-ldm7je/index.html.
16 Michela Wrong, *It's Our Turn to Eat: The Story of a Kenyan Whistle-Blower* (London: HarperCollins, 2009), pp. 41-42.
17 Ronald Slye, *The Kenyan TJRC: An Outsider's View from the Inside* (Cambridge: Cambridge University Press, 2018), p. 65.
18 F. Daniel Hidalgo and Simeon Nichter, "Voter-Buying: Shaping the Electorate through Clientelism," *American Journal of Political Science* (version of record online August 6, 2015). Website: www.mit.edu/~dhidalgo/papers/Voter_Buying.pdf.
19 "Report of the Judicial Commission Appointed to Inquire into Tribal Clashes in Kenya" (1999), p. 57.
20 Michael Kniss, "Walking Kenya Back from the Brink: A Micro-Level Study of Horizontal Inequity and Civil Conflict Prevention," CISSM working paper (2010).

ictj chapisho fupi

Tume Ya "Building Bridges" Yaweza Kuvunja Michakacho Ya Ufisadi Na Vurugu Za Kisiasa Nchini Kenya?

kwa kesi katika mahakama ya Jinai ya Kimataifa (ICC),[21] kufuatiwa na uondoaji wa uchunguzi uliochukuliwa na kiongozi wa mashtaka wa ICC na ukosefu wa uwajibikaji humu nchini juu ya ghasia zilizotokea mnamo 2007 na 2008 vinaweza kuelezea kwa nini uchaguzi mkuu wa 2017 ulisababisha vurugu kuanza tena.

Kwa Wakenya wengi, ugatuzi umekuwa njia ya kushughulikia kutwengwa na ukosefu wa usawa wa kihistoria katika usambazaji wa rasilimali za serikali. Kwa kweli, Katiba ya Kenya ya 2010 ilihitaji ugatuzi kama njia ya kurekebisha mifumo ya kutwengwa na kukomesha mfumo wa siasa wa "mshindi hupata zote" nchini Kenya. Lakini hatua hii pia imeishia kuunda nafasi zaidi za nyadhifa serikalini gatuzi na kwa hivyo imeongeza fursa za mashindano ya kisiasa yenye vurugu. Kama ilivyoashiriwa na Tume ya Kitaifa ya Ushirikiano na Maridhiano (NCIC),[22] tangu ugatuzi kumekuwa na kuongezeka kwa "…viwango vya siasa kukuza na kuibuka tena kwa vikundi vya wahalifu vilivyohusika na vurugu katika maeneo tofauti ya nchi kabla, wakati wa na baada ya kipindi cha uchaguzi."[23]

Wanasiasa wanaowania kuchanguliwa tena hapo awali walikuwa wanazua vurugu za kisiasa, huku wakiongezea wizi wa pesa za umma katika kipindi cha kabla ya uchaguzi ili kufadhili ununuzi wa kura na madai yanayohusiana na urejeshi. Sasa, vikundi vya upinzani vinazidi kugeukia vurugu katika harakati za kuwazuia wanasiasa wanaowania viti vya kisiasa tena kutorudi mamlakani. Kusajili, kufunza, na kutunza magenge kunahitaji pesa nyingi ambazo hazipatikani kwa wapinzani isipokuwa wakati wanapata nafasi, na kupora, rasilimali za umma.

Ukosefu wa ajira kwa vijana, ambao idadi yao inaendelea kuongezeka, imenukuliwa kama sababu inayoweza kudhoofisha mshikamano wa kijamii na utulivu wa kisiasa.[24] Watajika wa kisiasa mara nyingi huelekea kuhamasisha vijana wasio na kazi ili kuzua chuki na kuchochea vurugu. Kutoka kwa Mkutano wa Umoja wa Afrika uliyofanyika huko Addis Ababa, Ethiopia, mnamo Januari 2009 ambao ulitangaza 2009 hadi 2018 kuwa "Mwongo wa Vijana wa Kiafrika," Kenya ilifufua Huduma ya Kitaifa ya Vijana (NYS) na mipango ya uwezeshaji iliyonuiwa kuwapa wanaohitimu stadi zinazohitajika kujikimu kimaisha au kujipatia kipato.[25] La kusikitisha ni kuwa, ufadhili wa miradi ya NYS-ambayo inapaswa kuchangia sana kutumia nguvu zao nyingi, ubunifu, na talanta za ujana kama ufunguo wa ustawi wa maisha ya usoni — imeishia pia kuibiwa kwa kiasi kikubwa

21 In March 2010, the prosecutor of the ICC opened an investigation involving crimes against humanity that took place during the 2007–2008 post-election violence in Kenya. Six Kenyans were subject to the investigation: now-president Uhuru Kenyatta, now–deputy president William Ruto Mohammed, Hussein Ali, Henry Kosgey, Francis Muthaura, and Joshua Sang. In 2011, charges were withdrawn involving Kenyatta and were not confirmed with respect to Muthaura and Ali, due to insufficient evidence. See the ICC's fact sheet here: www.icc-cpi.int/kenya/kenyatta. With respect to Ruto and Sang (and Kosgey implicated with them), the ICC terminated the case in 2016 after the charges were vacated. See the ICC's fact sheet here: www.icc-cpi.int/kenya/rutosang. For ICTJ's view on what should happen with the termination of these cases, see Christopher Gitari, "After Collapse of ICC's Ruto and Sang Case, Kenya Must Prioritize Reparations and National Prosecutions" (2016). Website: www.ictj.org/news/icc-ruto-sang-kenya-reparations-victims.

22 The NCIC was created through the National Cohesion and Integration Act No. 12 of 2008. According to its website, "the establishment of NCIC recognized the need for a national institution to promote national identity and values, mitigate ethno-political competition and ethnically motivated violence, eliminate discrimination on ethnic, racial and religious basis and promote national reconciliation and healing." Website: www.cohesion.or.ke/index.php/about-us/ncic-at-a-glance.

23 National Cohesion and Integration Commission Kenya, "NCIC Launches a Report on Organized Gangs" (March 2018). Website: www.cohesion.or.ke/index.php/media-center/latest-news/227-ncic-launches-a-report-on-organized-gangs.

24 "High unemployment, particularly youth unemployment, appears to increase the risk of violence": World Bank, World Development Report 2011: Conflict, Security, and Development (Washington, DC: World Bank, 2011), Pg. 78 Website: http://siteresources.worldbank.org/INTWDRS/Resources/WDR2011_Full_Text.pdf.

25 African Union Commission, "African Youth Decade, 2009–2018 Plan of Action: Accelerating Youth Empowerment for Sustainable Development" (May 2011).

Tume Ya "Building Bridges" Yaweza Kuvunja Michakacho Ya Ufisadi Na Vurugu Za Kisiasa Nchini Kenya?

kupitia ufisadi. Kilichonuiwa kuwa suluhisho la ufisadi na ghasia za kisiasa zilizochangiwa na ufisadi badala yake kinaweza kuwa chanzo cha ufisadi zaidi na ghasia za kisiasa.

Kuendeleza Udhalimu wa Ardhi kupitia Ufisadi

Serikali zilizofuatia baada ya ukoloni hazikutengua hali ya kukandamiza iliyosababishwa na wakoloni Kenya wala hazikuchukua hatua madhubuti kusuluhisha ukosefu wa usawa ambao wakoloni walisababisha, hasa ukosefu wa usawa wa umiliki wa ardhi kati ya jamii kikabila za Kenya na jamii kwa jumla. Kulingana na mojawapo ya ushahidi uliotolewa katika vikao vya TJRC zilizolenga kiini cha kutengwa kwa kiuchumi nchini Kenya:

> Kulikuwa na muundo wa serikali ya kikoloni yenyewe na mikakati ambayo iliwekwa kupendelea vikundi fulani dhidi ya vingine. Walakini, kukamilika kwa kipindi cha ukoloni, masuala ya ukosefu wa usawa hayakuisha tu na ukoloni. La kusikitisha ni kuwa, serikali ya kwanza iliyochukua mamlaka ilichagua kuendelea na baadhi ya sera hizo katika kipindi cha baada ya uhuru ambayo haikuongeza tu bali, katika hali nyingi, ilizidisha ukosefu wa usawa.[26]

Kuhamishwa kwa lazima kwa jamii asilia wakati wa ukoloni kulisababisha jamii nyingi hizi kukosa ardhi na hivo basi kuwaacha maskini; kutengwa huku kwa kiwango kikubwa kutokana, na pia usambazaji usio na usawa wa ardhi uliendelea kutekelezwa baada ya uhuru, huku wanasiasa tajika wa Kiafrika baada ya Kenya kujitawala wakichukua nyadhifa za wakoloni.[27] Katika ripoti yake, TJRC ilibaini uhusiano kati ya ukosefu wa haki katika kumiliki ardhi, kwa upande mmoja, na sakata ya vurugu zinazohusiana na uchaguzi nchini Kenya, kwa upande mwingine.[28] Pia iliripoti kwamba zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya taarifa na kumbukumbu walizopokea kutoka kwa umma ziligusia juu ya migogoro ya ardhi. Mwongo kabla ya TJRC, mnamo 2004, Tume ya Ardhi ya Ndung'u iliundwa kama "tume ya uchunguzi katika ugawaji haramu wa ardhi ya umma."[29] Kulingana na Tume ya Ndung'u, " zaidi ya hati 200,000 zisizo halali au zisizo za kawaida ziliundwa na kusajiliwa kati ya 1963 na 2002."[30]

Wakenya walikuwa na matumaini makubwa na matarajio kwamba baada ya kupata uhuru kutoka kwa wakoloni, ukosefu wa haki ya ardhi ungekoma. Miongoni mwa faida nyingine, "…uhuru ulimaanisha kurudi katika mashamba au ardhi ambazo walikuwa wamefuruswa kwa nguvu na ambazo walikuwa wamenyang'anywa ili kuwapa nafasi walowezi wa Uingereza."[31] Walakini, leo, sio idadi ndogo tu ya wanasiasa na watajika wa kiuchumi waomiliki sehemu kubwa ya ardhi vijijini na mijini, lakini kuendelea kwa unyakuzi wa ardhi na viongozi wa kisiasa na wakuu wa serikali inamaanisha suala la ardhi litaendelea kuchochea vurugu za kisiasa."[32] Uundaji wa Tume ya Kitaifa ya Ardhi mnamo 2012 ilikuwa hatua katika mwelekeo unaofaa, lakini dhamira ya kisiasa na kujitolea kuunga mkono kwa dhati tume hiyo na pia kutoa rasilimali muhimu kwa ajili yake ili

26 TJRC Kenya, "Report of the Truth, Justice and Reconciliation Commission, Volume IIB" (2013), Pg. 20.
27 MatundaNyanchama, "Kenya: Roots of Conflict and Hope for the Future," speech made March 6, 2008, at Brock University, Ontario, Canada. Dr. Nyanchama is a respected leader of Kenya's diaspora.
28 TJRC Kenya, "Report of the Truth, Justice and Reconciliation Commission, Volume 2B" (2013), 341. Website: https://digitalcommons.law.seattleu.edu/tjrc-core/.
29 The commission's full report is available at http://kenyalaw.org/kl/fileadmin/CommissionReports/A_Report_of_the_Land_Commission_of_Inquiry_into_the_Illegal_or_Irregular_Allocation_of_Land_2004.pdf.
30 Zoe Flood, "Land Holds Key to Kenyan Rivalries," *Al-Jazeera*, March 4, 2013. Website: www.aljazeera.com/indepth/features/2013/03/20133413271622325 8.html.
31 TJRC Kenya, "Report of the Truth, Justice and Reconciliation Commission, Volume 1" (2013), p. ix. Website: https://digitalcommons.law.seattleu.edu/tjrc-core/
32 Luke M. Obala and Michael Mattingly, "Ethnicity, Corruption and Violence in Urban Land Conflict in Kenya," *Urban Studies* 51:13 (2014): 2735-2751.

kuiwezesha kutekeleza majukumu yake lazima ipaliliwe. Mipango ya sera kwa mara nyingi kumepuuza haja ya kushughulikia kiini cha malalamiko na migogoro inayohusiana na swala la mashamba au umiliki wa ardhi. Sheria za maana zilizoashiria kutekeleza vifungu vya katiba vimepuuza kusudi la katiba kushughulikia udhalimu wa ardhi wa kihistoria na wa sasa. Sera ya Ardhi ya Kitaifa bado haijaendeleshwa.

Ufisadi nchini Kenya, kwa kweli ni njia ya moja kwa moja ya kumiliki ardhi haramu, iwe kwa kunyakua ardhi ya umma au ya kibinafsi au kwa kubinafsisha au kupata ardhi inayomilikiwa na serikali kwa gharama kiasi au bila gharama. Kama ilivyowasilishwa na TJRC, "watu ambao ni mafisadi wanaweza kutumia umahiri wao duni na mamlaka yao kunyakua mali ya umma zaidi kama viwanja vya michezo, mashule, hospitali, nyumba za serikali, majengo na ardhi ya mahakama, na hivyo kunyima umma upataji na utumizi wa huduma muhimu za umma."[33] Kilichosemwa kwa busara hadharani kwa tume ya TJRC kuhusu ukosefu wa haki ya kumiliki ardhi kinabaki kuwa kweli sasa: "Kwa wale ambao hawawezi kupata mamlaka ya kisiasa, kutengwa kisiasa kutokana na umiliki wa ardhi kumezua chuki kubwa, haswa ambapo walinzi wa kisiasa na watawala ambao wanadhibiti umiliki wa ardhi wanaonekana kupendelea watu wa jamii zao."[34]

Kujifunza kutoka kwa Nchi Zingine

Nchini Colombia na Ufilipino, michakato ya haki ya mpito imechunguza utengaji wa kiuchumi na kijamii na vile vile ukosefu wa haki unaohusiana na ardhi ambao umesababisha miongo kadhaa ya vurugu za kisiasa na mizozo yenye kutumia silaha. Tofauti na Kenya, hata hivyo, Colombia ilitunga Sheria za Kuwafidia Waadhiriwa na Sheria ya Kurejesha Ardhi (Victims' Reparations and Land Restitution Law) mnamo 2011, ambayo imekuwa ikitekelezwa, licha ya ugumu wa ujuzi na kutokuwa na uhakika wa kisiasa unaohusika na hata kabla ya kuunda tume yake ya ukweli.[35] Huko Ufilipino, Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano (Truth, Justice and Reconciliation Commission) iliundwa kuchunguza sababu za ukiukaji na ukiukwaji wa haki za binadamu-ikiwa ni pamoja na kunyakuliwa kwa ardhi ya asili na kuhamishwa kwa jamii asilia- katika vita vya muda mrefu vya ukiri vilivyotekelezwa na vikundi vya kujitenga kusini mwa nchi yao. Majadiliano ya Tume hiyo sasa yatachukuliwa na kutekelezwa, miongoni mwa njia nyingine, kupitia sheria inayounda serikali ya kikanda inayojitegemea na mfumo tofauti wa kufuata hatua za haki za wakati wa mpito.[36]

Vile vile, nchi kama Ufilipino, mfumo wa ukiri wa Arabuni Tunisia, na Guatemala zimeonyesha kuwa hatua za haki za wakati wa mpito na njia za uchunguzi wa mseto zinaweza kutumiwa kufuatilia uwajibikaji kwa ufisadi, kurejesha mali ambayo inaweza kutumika kwa ulipaji wa fidia, na kisha kutumia zile mali kuwanufaisha wahasiriwa na maeneo yaliyotengwa. Wakati Kenya imefanya mchakato wa kutafuta ukweli ulioshughulikiwa na ufisadi, miongoni mwa ukiukaji mwingine, viongozi wake, pamoja na wale wanaohusika katika BBI, wamezungumzia ufisadi tu au kwa hiari, kupitia kile kinachoonekana kuwa kuhujumiwa kwa watu binafsi wasiounga mkono uongozi wa sasa. Kama nchi hizi zinavyoonyesha, hata hivyo, Kenya inaweza kufikiria kuunda

33 TJRC Kenya, "Report of the Truth, Justice and Reconciliation Commission, Volume 2B," p. 369.
34 Ibid.
35 See Cristián Correa, International Center for Transitional Justice, "From Principles to Practice Challenges of Implementing Reparations for Massive Violations in Colombia" (2015). Website: www.ictj.org/sites/default/files/ICTJ_Report_ColombiaReparationsChallenges_2015.pdf.
36 Antonio L. Colina IV, "Bangsamoro Law Seen to Heal Political, Historical Wounds," *Mindanews*, November 19, 2018. Website: www.mindanews.com/top-stories/2018/11/bangsamoro-law-seen-to-heal-political-historical-wounds/.

mfumo maalum na hata kuomba msaada wa kimataifa wa kuchunguza urejeshaji wa mali iliyoporwa na utaratibu wa mashtaka kukabiliana na ufisadi. Kenya inapaswa kushughulikia ukosefu wa haki unaohusiana na ardhi na utengwaji zaidi kwa kuwapa waKenya waliotengwa na wasio na ardhi ufikiaji endelevu na wa kudumu wa kuishi, ardhi, na rasilimali zinazotosheleza haki zao za kijamii na kiuchumi.

Kuenda Zaidi Ya "Ujenzi Wa Madaraja"

Chaguo lawahusika waku wa vyama vya kisiasa nchini Kenya kukabiliana na ufisadi kama suala kubwa kupitia mpango wa BBI, ikiambatana na juhudi kubwa za ukurugenzi wa Mashtaka ya Umma na ile ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai ya Kenya kuchunguza na kushtaki maafisa wa ngazi za juu kwa ufisadi,[37] inapaswa kuwa imehamasisha sana mtazamo wa umma kuhusu kujitolea kwa Kenya kupigana na ufisadi. Kila mwaka, shirika la Transparency International hutoa Kielelezo cha Ufahamu wa Ufisadi (Corruption Perception Index — CPI) kinacho orodhesha nchi kulingana na "mitazamo ya kiwango chake cha ufisadi kwenye sekta ya umma," kwa kuzingatia maoni kati ya wataalam na wafanyabiashara. CPI hutumia kiwango cha 0 hadi 100, ambapo 0 ni "mafisadi sana" na 100 ni "safi sana," na nchi zikiorodheshwa kulingana na maoni ya kuwa "chache" (1) kwa "mafisadi" zaidi (180).[38] Mnamo mwaka wa 2018, mwaka wa uzinduzi wa BBI, Kenya ilipata 27 kwa 100, ikichukua nafasi ya 144 kati ya nchi 180 na kupiga hatua moja chini kutoka mwaka uliopita.

Je! Ni sababu gani za mtazamo huu unaoendelea na kuzidi kuwa mbaya kati ya Wakenya, na kuja pamoja kwa rais Kenyatta na mhesimiwa Odinga kupitia kwa "handshake" kutaathiri ufisadi na maoni ya kuendelea kwake? Kwamba kuundwa kwa BBI na ujumuishaji wa ufisadi kati ya vipaumbele vyake ni hatua za hivi karibuni ni moja ya maelezo ya dhahiri. Lakini maelezo mengine ni wasiwasi mwingi juu wa kile kinachojulikana kama bado biashara nyingine ya wanasiasa tajika ambayo inachenga kiini au sababu za vurugu za kisiasa nchini Kenya kwa kukataa kuchukua hatua madhubuti kutekeleza mapendekezo yaliyoamurishwa na serikali, kama vile ya TJRC, ya kuwataka watu na taasisi zote kuwajibishwa juu ya ufisadi, ukosefu wa haki ya ardhi, na ukiukwaji wa haki za binadamu. Hii haimaanishi kwamba Wakenya hawawezi kufanya mradi wa BBI msingi wa kutetea uwajibikaji juu ya ufisadi na haki kwa waathiriwa wa dhuluma zinazotokana na vurugu za kisiasa. Lakini kwa kufanya hivyo, Wakenya hawapaswi kuridhika na matamko rasmi na ishara za kuwafanya wapunguze madai ya haki. Wanaweza na walipaswa kujifunza kutoka kwa kilichofanyika — au hakijafanya — kufuatia pendekezo la serikali la Fedha za Kurejesha Haki (Restorative Justice Fund (RJF): Baada ya Rais Kenyatta kutangaza kuunda mchango wa KES10 bilioni mwaka 2015,

37 Paul Ogemba, "DPP Seeks to Bank on Expunged Evidence in Kidero Graft Case," *The Standard*, September 24, 2019. Website: www.standardmedia.co.ke/article/2001343073/dpp-seeks-to-bank-on-expunged-evidence-in-kidero-graft-case; Faith Karanja, "EACC Found Huge Amounts of Cash in Nairobi Governor Evans Kidero's Account Suspicious," *The Standard*, March 16, 2016. Website: www.standardmedia.co.ke/article/2000195080/eacc-found-huge-amounts-of-cash-in-nairobi-governor-evans-kidero-s-account-suspicious; Macharia Gaitho, "Politicising War on Corruption Akin to Fanning Ethnic Violence," *Daily Nation*, December 11, 2018. Website: www.nation.co.ke/oped/opinion/Politicising-war-on-graft--akin-to-fanning-ethnic-violence/440808-4889638-ld-m7je/index.html; Gloria Aradi, "DPP: High Profile Graft Suspects Are Harassing Our Officers," *The Standard*, May 30. 2019. Website: www.standardmedia.co.ke/article/2001327741/.

38 Transparency International, Corruption Perceptions Index 2018. Website: www.transparency.org/cpi2018.

Tume Ya "Building Bridges" Yaweza Kuvunja Michakacho Ya Ufisadi Na Vurugu Za Kisiasa Nchini Kenya?

hakuna hatua yoyote muhimu ambayo imefanywa kutekeleza hatua za ulipaji wa fidia kama ilivyotarajiwa na TJRC katika matokeo na mapendekezo yake.[39]

Ijapokuwa Rais Kenyatta na Raila Odinga wameendelea kushutumu ufisadi, Wakenya bado hawajaona mafanikio dhidi ya kesi zenye hadhi kubwa ambazo zinaweza kutumika kama kizuizi na kukomesha kutokujali. Hii inatoa dhana kwamba watu hawa wenye kesi wamelindwa. Maafisa wa mahakama, wachunguzi, na waendesha mashtaka lazima wachukue jukumu lao kuhakikisha kwamba wale walio na hatia ya kuiba mali ya umma wameshtakiwa, na fedha ambazo zimeibwa kutafutwa na kurudishwa. Hali kadhalika, tabia ya kuficha au kuzifanya siri kampuni zilizosajiliwa inapaswa kukomeshwa, kwani imedhalilishwa kwa kuanzisha kampuni za kigumba ambazo hutumika kuiba fedha za umma na kupata kandarasi za gharama za juu ambazo hazitoi faida za kweli kwa umma, huku pesa zilizoibwa zikifichwa nchini zingine bila kupatikana.

Wakati lengo kwa vita dhidi ya ufisadi lvmeangazia wafanyikazi wa umma na viongozi wa sekta za kibinafsi, vinahitajika kupanuliwa na kuangaliwa kwa kina. Wananchi wa kawaida wanateseka zaidi wakati pesa zilizokusudiwa kwa maendeleo na utoaji wa huduma muhimu kama uzalishaji wa chakula, makazi, elimu, na huduma za afya huibwa kwa njia za ufisadi. Kuhusisha umma, na hasa vijana na wanawake ambao huumizwa zaidi na adhari za ufisadi kutaimarisha vita dhidi ya ufisadi zaidi. Toleo la kumi la Barometa ya Ufisadi Ulimwenguni-Afrika (Global Corruption Barometer-Africa), WaAfrika wengi wanahisi kwamba ufisadi umeongezeka nchini mwao, watu wengi pia wana jiamini kwa kuwa wanaweza kuchangia mabadiliko katika mapambano dhidi ya ufisadi — kwa hivyo kuna umuhimu wa kuwashirikisha.

Ni muhimu, kwa mfano, kuimarisha ulinzi wa wapiga mbiu na kuunda mifumo zaidi ambayo itawahimiza raia kutoa ripoti za ufisadi bila kuogopa kulipizwa. Matokeo yanayotia wasiwasi na ambayo yanapaswa kushtumiwa yanatokana na mahakama kuwaadhibu wapiga mbiu walioshtakiwa na watajika wakuu na wenye nguvu kisiasa kwa kile wanadai ni kuchafuliwa sifa kwa madai ya ufisadi.[40] Hali kadhalika, vyombo vya habari na asasi za kijamii hazifai kugandamizwa kwa kuiita serikali na kuihimiza kuwajibika kwa uhalifu wa kiuchumi na mengine ambayo huzindisha kutowajibika.

Kujitolea kisiasa ili kupigana na kukomesha ufisadi unahitajika kutekeleza sheria zilizopo na kuziunga mkono taasisi zinazoshughulikia ukosefu wa haki wa ardhi, mali iliyoibiwa, na vurugu za kisiasa nchini. Serikali inaweza kushughulikia dhuluma zinazohusiana na ukiukaji wa haki za ardhi kwa kutekeleza mapendekezo ya ripoti ya TJRC ya 2013 na vile vile ripoti ya Tume ya Ardhi ya Ndung'u ya 2004, kati ya ripoti nyingine za tume za zamani za uchunguzi. Kulingana na pale Kenya ilipo sasa katika vita dhidi ya ufisadi na kuzuia vurugu za kisiasa, hata kutoa fidia kwa waathiriwa na kurekebisha malalamiko yanayohusiana na ardhi za wizi na utengwaji, ni dhahiri kwamba ujenzi wa amani au 'madaraja' kati ya wataajika wakuu wa Kenya haitoshi.

39 To their credit, the Kenya attorney general's office has been drafting regulations to govern the RJF's implementation. ICTJ has provided input in this drafting process. These drafts, however, have not been approved as of the writing of this paper.

40 Jacob Ng'etich, "Ruling on Githongo Pushes the Bar on Whistleblowing," Standard, May 21, 2019. Website: www.standardmedia.co.ke/article/2001326509/ruling-on-githongo-pushes-the-bar-on-whistleblowing.

ictj chapisho fupi

ICTJ Justice Truth Dignity

The International Center for Transitional Justice works across society and borders to challenge the causes and address the consequences of massive human rights violations. We affirm victims' dignity, fight impunity, and promote responsive institutions in societies emerging from repressive rule or armed conflict as well as in established democracies where historical injustices or systemic abuse remain unresolved. For more information, visit **www.ictj.org**

ICTJ Kenya
Mtito Andei Apts. House No. C1
Mtito Andei Road
Nairobi, Kenya
Tel: +254 725 000958